

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Telegrams: "UTUMISHI", DAR ES SALAAM
Simu : +(255) 22 2118531-4
Fax No.: +(255) 22 2125299
E-mail: permsec@utumishi.go.tz



Utumishi na Utawala Bora,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P 2348,
11404 DAR ES SALAAM.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CDC.228/297/01/6

30 Mei, 2016

**WARAKA WA UTUMISHI NA. 1 WA MWAKA 2016 KUHUSU
UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA KIMKAKATI AJIRA ZA
WATAALAM WA KITANZANIA KATIKA TAASISI ZA
KIMATAIFA NA KIKANDA**

1.0 Utangulizi

1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Taasisi mbalimbali za Kimataifa na Kikanda. Faida zinazopatikana kutokana na nchi yetu kuwa mwanachama ni pamoja na kupata fursa mbalimbali zikiwemo ajira za Wataalam wa Kitanzania katika Taasisi hizo. Ajira hizi hutoa fursa kwa Wataalam hao kuongeza upeo, ujuzi na uzoefu katika nyanja mbalimbali. Uzoefu wanaoupata wataalam hawa hutumika kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi Serikalini pindi wanaporejea nchini baada ya kumaliza mikataba yao. Aidha, kuwepo kwa watanzania kwenye Taasisi hizi hususan katika nafasi muhimu kunasaidia kutetea masilahi ya nchi katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Vile vile mishahara na marupurupu mengine wanayolipwa huko huchangia katika kukuza pato la Taifa.

1.2 Katika kuhakikisha kuwa fursa za ajira za Wataalam wa Kitanzania katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda zinatumia vizuri kwa manufaa ya Taifa, Serikali ilitoa Waraka wa Utumishi Na. 9 wa mwaka 1992 uliohusu Utaratibu wa Kuajiri na Kutumia Vizuri Wataalam Wazalendo Nje na Ndani ya Utumishi wa Umma. Vile vile zimekuwapo jitihada za kufuatilia fursa za ajira zinazopatikana katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda; kutoa taarifa za nafasi za kazi zilizojitokeza; kuwahimiza Wataalam wa Kitanzania kujitokeza kuomba nafasi hizo; na inapowezekana, kutoa mafunzo kuhusu usaili kwa waombaji wa kazi kwenye nafasi hizo.

